

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA SABA

13 NOVEMBA, 2019



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

KIKAO CHA SABA – TAREHE 13 NOVEMBA, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuhusu:-

Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluocarbons (HFCS) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni (*Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances*); na

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu (*The Southern African Development*

*Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu:-

Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluocarbons (HFCs) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni (*Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances*); na

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu (*The Southern African Development Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development*).

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu:-

Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza Uzalishaji na

Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluocarbons (HFCS) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni (*Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances*); na

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu (*The Southern African Development Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development*).

### **WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Maelezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia (*Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization*).

### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia (*Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization*).

## **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia (*Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization*).

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **85. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (SAME MASHARIKI):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali inashirikiana na Hospitali ya Gonja chini ya KKKT na Hospitali hiyo inatoa huduma za upasuaji kwa Wagonjwa wengi kuliko Hospitali ya Wilaya ya Same. Aidha, Jimbo la Same Mashariki lenye Kata 14 lina Kituo kimoja tu cha Afya kilichoboreshwana na hivyo kusababisha msongamano wa Wagonjwa katika Hospitali ya Gonja:-

Je, ni lini Serikali itaongeza Madaktari katika Hospitali ya Gonja ili iweze kuhudumia Kata 9 ambazo Wagonjwa wake wanapata shida ya kusafiri umbali mrefu kufuata matibabu Hospitali ya Wilaya ya Same.

**86. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kata ya Mtama katika Manispaa ya Singida haina Kituo cha Afya kwa ajili ya kuwahudumia wakazi wake na Sera ya Serikali inaelekeza kila Kata kuwa na Kituo cha Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuifanya Zahanati ya Mtisi kuwa Kituo cha Afya, ambayo ujenzi wake umekuwa wa kusuasua kutokana na Serikali kutopeleka fedha za kutosha.



**87. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Kituo cha Afya Kidodi katika Wilaya ya Kilosa kitapatiwa Wafanyakazi wa kutosha.

**WIZARA YA MAJI:**

**88. MHESHIMIWA FRANK GEORGE MWAKAJOKA (TUNDUMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itafufua mradi mkubwa wa maji wa kutega maji safi na salama katika Kijiji cha Ukwile mradi ambao ulijengwa na Shirika la Reli (TAZARA) uliokuwa ukihudumia Wananchi wa Kata ya Mpemba na Katete.

**89. MHESHIMIWA HAJI KHATIB KAI (MICHEWENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Serikali ya Tanzania ilipata mkopo wa USD milioni 500 wenyewe masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maji katika Miji ikiwemo Zanzibar:-

Je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kuanza kwa miradi hiyo.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**90. MHESHIMIWA MARWA RYOBIA CHACHA (SERENGETI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Kampuni ya Tanzania Oxygen kwa muda wa takribani miaka 30 imehodhi eneo lenye maji ya moto lililopo Kata ya Majimoto Kijiji cha Majimoto katika Wilaya ya Serengeti:-

Je, Serikali ipo tayari kulitwaa eneo hilo na kuwarejeshea Wananchi kwa kuwa Kampuni hiyo ilishashindwa kuliendeleza.

**WIZARA YA KILIMO:**

**91. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Kuna Skimu ndogo na kubwa za umwagiliaji ambazo hazitumiki kama ilivyosanifiwa na kujengwa na nyingine zimekufa katika Wilaya za Moshi, Hai na Same Mkoani Kilimanjaro:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kufufua na kurejesha Skimu hizo zifanye kazi kama ilivyokusudiwa.

**92. MHESHIMIWA SAUL HENRY AMON (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Jimbo la Rungwe ni kati ya maeneo yenye ardhi yenye rutuba na inafaa sana kwa Kilimo cha maparachichi:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vitalu vya maparachichi ili Wananchi wapate miche kwa bei nafuu kwani bei ya sasa ya shilingi elfu tatu kwa mche kwa Mkulima wa kawaida ni ghali sana;

- (b) Kilimo cha maparachichi kinahitaji utaalamu ili kukidhi kiwango cha Kimataifa. Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza Wataalam wa Kilimo katika Jimbo la Rungwe.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**93. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

- (a) Je, ni Mikataba mingapi ya Kimataifa ambayo nchi imesaini lakini haijaridhiwa;
- (b) Je, kuna athari zozote kwa nchi kutoridhia Mikataba ambayo tayari nchi imesaini.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**94. MHESHIMIWA ANTHONY CALIST KOMU (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Kiboroloni, Kikarara, Kidia mpaka Tsuduni yeny urefu wa Kilometra 10.8 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

**95. MHESHIMIWA DKT. SHUKURU JUMANNE KAWAMBWA (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ujenzi wa Barabara ya Makofia – Mlandizi kwa kiwango cha lami uko katika llani za Uchaguzi za CCM za miaka 2005, 2010 na 2015:-

Je, ni lini Barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

**96. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ipo ahadi ya Mhe. Rais juu ya ujenzi wa barabara ya kutoka Samuye – Choma – Zia – Nkinga – Simbo hadi Puge inayokadiriwa kuwa na urefu wa km. 100:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

## **97. MHESHIMIWA JANET ZEBEDAYO MBENE (ILEJE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Michezo ya kubahatisha inaingiza pato kwa Taifa lakini ina athari kubwa za kimaadili na kisaikolojia kama ilivyo kwenye dawa za kulevyaa ikiwa haitaangaliwa kwa umakini:-

- (a) Je, Serikali imechukua tahadhari zipy kuhakikisha kuwa michezo hii inashirikisha watu wenyewe ufahamu wa athari za kutegemea michezo hii hali inayoweza kuwaletea athari kubwa za kiuchumi, kijamii, hadi ndani ya familia na Taifa kwa ujumla;
- (b) Je, Serikali inaweza kuwatambua na kuwafuatilia wachezeshaji wote wa michezo hii ya kubahatisha.

## **98. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Kumekuwa na Malalamiko toka kwa Wafanyabiashara kwamba tozo na kodi zimezidi na kusababisha kukosa faida au kusababisha mfumuko wa bei pamoja na upungufu wa Wateja:-

Je, ni lini Serikali itaondoa kero hizo ili kukuza biashara.

### **WIZARA YA NISHATI:**

#### **99. MHESHIMIWA ALLY SEIF UNGANDO (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Wananchi wa Jimbo la Kibiti katika maeneo yaliyofikiwa na umeme baadhi yao wamekuwa na adha kubwa kwa kuwa wamelipia nguzo na mita lakini TANESCO wameshindwa kutimiza wajibu wao:-

- (a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha TANESCO kushindwa kutimiza wajibu wao;
- (b) Je, ni lini Wananchi hao watapelekewa huduma ya umeme ikiwa tayari wameshalipia.

### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **MAAZIMIO:**

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluocarbons (HFCS) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu

Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni (*Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances*); na

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu (*The Southern African Development Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development*).

#### **WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia (*Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization*).

DODOMA

13 NOVEMBA, 2019

S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE